

## MKATABA WA MAUZIANO YA SHAMBA

MKATABA HUU umefanyika leo hii tarehe...<sup>30</sup>..... mwezi Disemba 2022

### KATI YA

**Bi. TAMAL JOSEPH MWASONGOLE** wa S.L.P 2839 Nyamhongolo, Ilemela **MWANZA** simu 0744678522 **MWANZA** ambaye katika mkataba huu ataitwa **Muuzaji**) kwa upande mwingine.

### NA

**CHENLIN INVESTMENTS CO.LIMITED** wa S.L.P 2839 Mwanza (ambaye katika mkataba huu ataitwa **mnunuzi**) kwa upande mmoja.

**KWA KUWA muuzaji** ni Mmiliki halali wa shamba lililoko kitongoji cha **Ihala** kijiji wa **IGEKEMAJA** kata ya **KISESA** Wilaya ya **MAGU** Jijini Mwanza likiwa na ukubwa wa mita za mraba 30,000, na yuko tayari kuliuzwa shamba hilo.

**NA KWA KUWA mnunuzi** amekagua na kuridhika na shamba hilo na amekubali kununua shamba hilo kwa makubaliano yaliyomo katika mkataba huu.

### HIVYO BASI, MKATABA HUU UNASHUHUDIA KAMA IFUATAVYO: -

1. Kwamba, **muuzaji** anamuuzia **mnunuzi** shamba tajwa hapo juu, ambalo maelezo yake yamewekwa ndani ya mkataba huu kwa hiari yake bila kushawishiwa, na **mnunuzi** ameridhia kununua shamba hilo.
2. Kwamba, bei ya mauziano iliyokubalika ni kiasi cha shilingi za **Kitanzania milioni mia moja (T.shs. 100,000,000/=)** tu, kiasi ambacho kitalipwa kwa awamu moja.
3. Kwamba, **Muuzaji** anauza shamba hilo kwa kufuata sheria za nchi na wakati wa mkataba huu, hakuna pingamizi lolote la kisheria lililopo kuzuia uuzaji huo.

### KWA MAKUBALIANO HAYA PANDE ZOTE ZINAWEKA SAINI ZAO KATIKA TAREHE, MWEZI NA MWAKA KAMA INAVYOONEKANA HAPA CHINI: -

**UMESAINIWA na KUTOLEWA** hapa  
**MWANZA na TAMAL JOSEPH  
MWASONGOLE**

Ambao nawafahamu binafsi /  
Wametambulishwa kwangu na .....  
.....ambaye namfahamu leo  
hii tarehe <sup>30</sup>.....mwezi Disemba, 2022

T. Joseph  
.....  
**TAMAL JOSEPH MWASONGOLE  
(MUUZAJI)**



**MBELE YANGU**

JINA: ..REHEMA M. MATENGU  
SAINI: ..~~REHEMA~~  
ANUANI: ..1744  
SIFA: ..WAKILI



UMETIWA LAKIRI/MUHURI na KUTOLEWA  
Hapa MWANZA na CHENLIN INVESTMENT  
CO LIMITED  
Leo hii tarehe. ~~30<sup>th</sup>~~ mwezi. ~~Disember~~ 2022

CHENLIN INVESTMENTS Co LIMITED  
P.O. Box 2839 MWANZA  
~~DATE 30/12/2022~~  
LAKIRI/MUHURI

\* JINA: ..LIN Zhu Xiang  
SAINI: ..林若萍  
ANUANI: ..2839. MWANZA.  
SIFA: ..MKURU (ENZI)

JINA: ..SHEBA GERALD  
SAINI: ..~~Sheba~~  
ANUANI: ..2839 MWANZA.  
SIFA: ..AFISA RASULIMALI  
WATU.